# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TISA

## KIKAO CHA NANE

**09 NOVEMBA, 2022**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA TISA

## KIKAO CHA NANE – TAREHE 09 NOVEMBA, 2022

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**107. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni Mikoa mingapi, Wilaya, Vijiji na Vitongoji wameunda Kamati za Watu Wenye Ulemavu.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**108. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini mkakati wa Serikali kujenga chumba cha upasuaji kwa ajili ya Wajawazito katika Kituo cha Afya cha Itaka Wilayani Mbozi.

**109. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Vituo vya Afya vya Rukaragata na Nemba vitapewa vifaa vya upasuaji.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**110. MHESHIMIWA RASHID ABDALLA RASHID (KIWANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni lini Serikali itaviwezesha vikundi vya uhifadhi mazingira Vijiji vya Chwaka, Kiwani, Jundamiti, Mwambe, Nanguji na Kendwa.

**WIZARA YA MAJI:**

**111. MHESHIMIWA LUCY JOHN SABU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza magari RUWASA – Simiyu ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**112. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, ni lini Serikali itaajiri Maafisa Habari katika Balozi zetu ili kutangaza nchi na vivutio mbalimbali.

**WIZARA YA KILIMO:**

**113. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufikisha Mbegu za Soya kwa Wakulima wa Jimbo la Newala Vijijini hasa Kata za Tarafa ya Chilangala.

## WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

**114. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali inakusanya kiasi gani cha asilimia 5 ya zawadi ya Washindi wa mchezo ya kubashiri na kimechangia kiasi gani kukuza michezo.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**115. MHESHIMIWA CHARLES JOHN MWIJAGE (MULEBA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kwa nini katika Tarafa ya Kamachumu Mlalamikaji hulazimishwa kumsafirisha Mahabusu kwenda na kurudi rumande.

**116. MHESHIMIWA ASYA SHARIF OMAR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati katika Kituo cha Polisi Matangatuani Wilaya ya Micheweni.

**117. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Sheria ya Kampuni Binafsi za Ulinzi.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**118. MHESHIMIWA SALIM ALAUDIN HASHAM (ULANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itafungua barabara ya kimkakati inayotoka Mahenge mpaka Liwale kupitia Malinyi, Mlimba, Njombe na Songea.

**119. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati reli ya TAZARA.

**120. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Choma – Ziba – Nkinga hadi Puge.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**121. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Ndaki ya Sayansi ya Afya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Mamlaka ya Mji wa Mbalizi.

**122. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR (NYANGH'WALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Chuo cha VETA Nyangh'wale.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**123. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa mpaka kati ya Wananchi wa Kata ya Itaka na Nambinzo na TFS kuhusiana na Pori la Hifadhi Isalalo.

**124. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mkakati gani kudhibiti Tembo wanaovamia Vijiji vya Doroto, Kitaraka, Kamenyanga, Gurungu, Muhanga na Njirii.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**125. MHESHIMIWA JULIANA DIDAS MASABURI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa Vichanja vya kuanikia Dagaa Wanawake Wajasiriamali wa Mkoa wa Mara.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**126. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano ya simu katika Kata za Karitu na Ikindwa – Bukene.

## III. KAMATI YA MIPANGO:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka 2023/2024 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc*** |
| **09 NOVEMBA, 2022** | **KATIBU WA BUNGE** |